# MAFUNDISHO YA BIBILIA

# KWA WATOTO WA

# KANISA LA ELOHIM (C. O. G)

# SIKU YA SABA (7TH DAY)

# ROBO YA TATU

# 2019
# JULAI, AGOSTI, SEPTEMBA

**KUTUMIWA NA BIBLIA**

**TUMA MAOMBI YOTE KWA**


**3RD ANGEL MESSENGER**

**S. L. P 9774 NAKURU**

**3rdangelmessenger@gmail.com**

**SIMU: +254 721576325 / +254 704590649**


-------------------------------------------------------

## SOMO LA WATOTO LA JULAI 6, 2019

### UTAKATIFU

**Somo kuu: Isaya 5:16-24**
**Fungu la kukariri: I Petero 1:16**

1. Maandiko yameeleza vipi kuhusu Elohim? Isaya 43:15
2. Nini kilihitajika kwa Wana wa Israeli ili wawe taifa takatifu? Kutoka 19:5-6
3. Makao ya Elohim yako vipi? Zaburi 68:5

4. Mtu mwenye pepo mchafu alinena vipi kuhusu Masihi? Mariko 1:23-24
5. Tumeshauriwa vipi kuhusu utakatifu? 1 Petero 1:15-16
6. Je,imani tunayoiyamini yafaa kuwa takatifu? Yuda 1:20
7. Yerusalemu mpya inayoshuka kutoka mbinguni imenenwa vipi? Ufunuo 21:2,21:10

## SOMO LA WATOTO LA JULAI 13, 2019

## AMRI

**Somo kuu : Kumbukumbu la torati 5:1-22**
**Fungu la kukariri : Ufunuo 14:12**

1. Nani alipeana amri kumi? Kutoka 20:1-4
2. Nani aliziandika amri kumi? Kutoka 31:18
3. Je,mwokozi wetu alizitupilia mbali amri kumi alipokuja ulimwenguni? Mathayo 5:17-18
4. Tukizitunza amri kumi, je tutapata uzima wa milele? Mathayo 19:16-17
5. Je tumeruhusiwa kuzivunja baadhi ya amri kumi? Yakobo 2:10-11
6. Nani wataruhusiwa katika mji ule mtakatifu? Ufunuo 22:14
7. Nani watakatifu? Ufunuo 14:12

## SOMO LA WATOTO LA JULAI 20, 2019

## DAUDI

**Somo kuu: 1 Samueli 16:1-13**
**Fungu la kukariri: Zaburi 78:70**

1. Nani alikuwa baba yake Daudi? Ruthu 4:22
2. Ni nabii yupi alimumwagia mafuta Daudi awe Mfalme? 1 Samueli 16:13
3. Je,Elohim alifanya agano na Daudi? Zaburi 89:3
4. Je,Masihi amenenwa kama mwana wa Daudi? Mathayo 1:1
5. Mtume Petero alinena vipi kuhusu Daudi? Matendo ya Mitume 2:29-34
6. Je,Masihi atatawala katika kiti cha Daudi? Luka 1:32
7. Yohana yule wa Ufunuo alinena vipi kuhusu Masihi akimlinganisha na Daudi? Ufunuo 22:16

## SOMO LA WATOTO LA JULAI 27, 2019

## MAPIGO KATIKA NCHI YA MISRI

**Somo kuu: Kutoka 7:1-25**
**Fungu la kukariri: Kutoka 7:9**

1. Kwa nini Elohim aliwaadhibu Wamisiri kwa Mapigo? Kutoka 7:15
2. Elohim alinena vipi kuhusu moyo wa Farao wakati wa mapigo? Kutoka 7:3
3. Muujiza wa Kwanza kwa Farao kutoka kwa Musa ulikuwa upi? Kutoka 7:9-10

4. Je,waganga wa Misiri pia walifanya muujiza kama wa Musa? Kutoka 7:11-12
5. Pigo la Kwanza lilikuwa lipi? Kutoka 7:19-21
6. Wakati pigo la chawa liliwafikia Wamisiri, waganga waliweza kufanya muujiza huo? Kutoka 8:17-19
7. Pigo la mwisho lilikuwa lipi katika nchi ya Misiri? Kutoka 12:29-31

## SOMO LA WATOTO LA AGOSTI 3, 2019

## MANABII

**Somo Kuu: 1 Wafalme 18:1-46**
**Fungu la kukariri : Amosi 3:7**

1. Nani alikuwa nabii wa Kwanza kutabiri kuhusu kurudi mara ya pili kwa Masashi? Yuda 1:14
2. Je,Elohim atafanya kitu duniani kabla ya kuwafunilia manabii wake? Amosi 3:7
3. Je,tuko na manabii waongo? Yeremia 14:14,5:31,Mathayo 24:11,24:24
4. Katika maandiko tuko na unabii uliotabiriwa na kutimizwa? Mika 5:2 patanisha na Mathayo 2:1
5. Je,kulikuwa na manabii wakati wa mitume? Matendo ya mitume 13:1
6. Ni ahadi gani ya unabii tumeahidiwa? Yoeli 2:28
7. Je,tumeshauriwa tusome maneno ya unabii? Ufunuo 1:3

## SOMO LA WATOTO LA AGOSTI 10, 2019

## KIFO

**Somo kuu: Mwanzo 3:1-19**
**Fungu la kukariri: Ahibirania 9:27**

1. Nani alikuwa Mtu wa Kwanza kupatana na mauti? Mwanzo 4:8
2. Alipokufa alienda wapi? Mwanzo 4:10-11 patanisha na 3:19
3. Je,kuna kumbukumbu yeyote katika kifo? Zaburi 6:5
4. Ayubu amenena vipi kuhusu kifo? Ayubu 10:22
5. Nini malipo ya dhambi? Warumi 6:23
6. Je,Masihi alishinda kifo? Ahibirania 2:14-15
7. Je,kuna kifo cha pili? Ufunuo 21:8

## SOMO LA WATOTO LA AGOSTI 17, 2019

## UFUFUO

**Somo kuu: Ufunuo 20:1-15**
**Fungu la kukariri: Ufunuo 20:5**

1. Kuna ufufuo mara ngapi? Ufunuo 20:5,20:13
2. Je,kuna ufufuo wa wenye haki? Luka 14:14
3. Je,kutakuwa na ndoa baada ya kufufuka? Luka 20:35-36
4. Je,tumeshauriwa tufunze mafundisho ya ufufuo? Ahibirania 6:2
5. Ni kiasi gani cha muda kati ya ufufuo wa Kwanza na wa pili? Ufunuo 20:5
6. Nani watatawala na Masihi? Ufunuo 20:6
7. Je,nabii Isaya alitabiri kuhusu ufufuo?

## SOMO LA WATOTO LA AGOSTI 24, 2019

## MUSA

**Somo kuu: Kutoka 2:1-25**
**Fungu la kukariri: Kutoka 2:10**

1. Nini maana ya Jina Musa? Kutoka 2:1-2
2. Ni kutoka kabila lipi wazazi wa Musa walitokea? Kutoka 2:1-2
3. Musa alikimbilia wapi alipopotea Misiri? Kutoka 2:15
4. Mke wa Musa kutoka kuhani wa midiani aliitwa vipi? Kutoka 2:21
5. Mwanawe aliitwa vipi? Kutoka 2:22
6. Jina la babaye Musa lilikuwa lipi? Kutoka 6:20
7. Je Musa alikuwa mtu mnyenyekevu? Hesabu 12:3

## SOMO LA WATOTO LA AGOSTI 31, 2019

## KUFUATA NYAYO ZA MASIHI

**Somo kuu: Afilipi 2:1-15**
**Fungu la kukariri: 1 Wakorintho 11:1**

1. Maisha ya Masihi yalikuwa vipi hapa ulimwenguni? Afilipi 2:5-8
2. Je tumeshauriwa tumuige? 1 Wakorintho 11:1
3. Je alikuwa anawatii wazazi wake na Elohim pia? Luka 2:52
4. Je wakati Masihi alipokuwa hapa ulimwenguni alijilipishia kisasi? 1 Petero 2:23
5. Tumeambiwa vipi kuhusu kujilipishia kisasi? Warumi 12:19
6. Ulimwengu utajua vipi ya kwamba sisi tu wafuasi wa Masihi? Yohana 13:35
7. Tukimpenda Masihi tutafanya nini? Yohana 14:15

## SOMO LA WATOTO LA SEPTEMBA 7, 2019

## MSAMAHA

**Somo kuu: Mathayo 18:21-35**
**Fungu la kukariri: Mathayo 18:21-22**

1. Masihi alipowafunza wanafunzi wake maombi, je aliwafunza kuomba msamaha? Mathayo 6:12
2. Tukisamehea ambao wametukosea, je Elohim atatusamehea? Mathayo 6:14
3. Tusipowasamehe ambao wametukosea, je Elohim atatusamehea? Mathayo 6:15
4. Paulo ametushauri vipi kuhusu Msamaha? Waefeso 4:32
5. Mwandishi wa Zaburi amenena vipi kuhusu Msamaha? Zaburi 130:4,103:3
6. Je Danieli aliomba msamaha kwa niaba ya watu wao? Danieli 9:18-19
7. Ni kwa nani tumepata Msamaha? Wakolosai 1:14,Waefeso 1:7

## SOMO LA WATOTO LA SEPTEMBA 14, 2019

## UPENDO

**Somo kuu: 1 Wakorintho 13:1-13**
**Fungu la kukariri: 1 Wakorintho 13:13**

1. Ni kwa njia gani twajua Elohim anampenda kila Mtu? Yohana 3:16
2. Twaweza kuonyesha upendo wetu vipi kwa Masihi na Elohim? Yohana 14:15
3. Je upendo ni amri? Yohana 15:12
4. Elohim alionyesha vipi upendo wake kwetu sisi tulipokuwa watenda dhambi? Warumi 5:8
5. Je upendo ni tunda la roho? Wagalatia 5:22
6. Ni upendo gani Elohim ametupa sisi? 1 Yohana 3:1
7. Je Elohim anawakemea awapendeo? Ufunuo 3:19

## SOMO LA WATOTO LA SEPTEMBA 21, 2019

## KITABU CHA UFUNUO

**Somo kuu: Ufunuo 1:1-20**
**Fungu la kukariri: Ufunuo 1:1**

1. Nani mwandishi wa kitabu cha Ufunuo? Ufunuo 1:1
2. Kuna baraka ya kusoma Ufunuo? Ufunuo 1:3
3. Nani alionyeshwa Yerusalemu mpya ikishuka kutoka mbinguni? Ufunuo 21:2
4. Je Yohana alionyeshwa mapigo ambayo yataupiga ulimwengu? Ufunuo 9 na 16
5. Ili kuepekuna na mapigo dunia imeshauriwa vipi? Ufunuo 14:9-10 na 18:4
6. Je tumekatazwa kuongeza chochote katika kitabu cha Ufunuo? Ufunuo 22:18
7. Tumenenewa vipi kuhusu malipo katika kitabu cha Ufunuo? Ufunuo 22:12

## SOMO LA WATOTO LA SEPTEMBA 28, 2019

## NUHU

**Somo kuu: Mwanzo 6:1-22**

**Fungu la kukariri: Mwanzo 6:8**

1. Nani alikuwa baba yake Nuhu? Mwanzo 5:28-29.
2. Elohim alipoona uovu wa mwanadamu umezidi katika Dunia, aliamua kufanya nini? Mwanzo 6:5-7.
3. Je, Nuhu alijiweko katika uovu wa wanadamu katika Dunia? Mwanzo 6:9
4. Ni kwa njia ipi Elohim alimchagua? Mwanzo 6:8
5. Ni nini Elohim alimwambia ajenge ili apate kuokolewa na uharibifu ambao ungepata Dunia? Mwanzo 6:13-14
6. Kando na yeye ni nani wengine waliokolewa na Elohim wakati wa kuharibiwa kwa Dunia? Mwanzo 8:16,18
7. Petero alinena vipi kuhusu Nuhu? 2 Petero 2:5